

Konde la Soani ni nini?

Soani/konde la Soani ni mji uliokuwa Misri, upande wa mashariki mwa bonde la mto Nile, tazama picha juu. Hili ndio eneo ambalo Musa alionyesha miujiza yote ya Mungu kwa Farao, pale alipomtaka awaaachie huru wana wa Israeli akakataa.

Hivi ni baadhi ya vifungu vinavyoelezea Neno hilo.

Zaburi 78:11 “Wakayasahau matendo yake, Na mambo yake ya ajabu aliyowaonyesha.

12 Mbele ya baba zao alifanya mambo ya ajabu, Katika nchi ya Misri, konde la Soani.

13 Aliipasua bahari akawavusha; Aliyasimamisha maji mfano wa chungu”.

Zaburi 78:42 "Hawakuukumbuka mkono wake, Wala siku ile alipowakomboa na mtesi.

43 Alivyoziweka ishara zake katika Misri, Na miujiza yake katika konde la Soani.

44 Aligeuza damu mito yao, Na vijito wasipate kunywa".

Hesabu 13:22 "Wakapanda katika Negebu, wakafika Hebroni; na Ahimani, na Sheshai, na Talmi, wana wa Anaki, walikuwako huko. Nao Hebroni ulijengwa miaka saba kabla ya Soani wa Misri".

Vifungu vingine ni Isaya 19:11,13, Ezeieli 30:14.

Tazama chini maana ya maeneo mengine katika biblia.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255 789001312

Mada Nyinginezo:

Mto Frati upo nchi gani, Umuhimu wake katika biblia ni upi?

WAKATI WA BWANA KUKUVUSHA, NI LAZIMA ARUHUSU JESHI LA ADUI KUNYANYUKA.

PARAPANDA ITALIA.

NAO WALIOKUWA WAMEKUSUDIWA UZIMA WA MILELE WAKAAMINI.

RUDI KUMPA MUNGU UTUKUFU.

UFUNUO: Mlango wa 19

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp